



TAFIRI yateketeza dhana za uvuvi haramu

Na Mathias Marwa, MARA

TAASISI ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), kupitia mradi ju-muishi wa jamii katika usimamizi wa uvuvi kwenye ardhioevu ya Mara imeteketeza nyavu za uvuvi haramu zilizosalimishwa na wavuvi zaidi ya 51 kutoka wilayani Ranya mkoani hapa na kukabidhiwa nyavu halali kwa ajili ya kuen-deleza shughuli za uvuvi.

Uteketezaji wa nyavu hizo pamoja na utolewaji wa nyavu halali umeongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Ranya, Juma Chikota, chini ya usimamizi wa TAFIRI, Mkoa wa Mwanza kwa ufadhilli wa Shirika la Darwin Initiative la Uingereza kwa lengo la kuiamarisha uhifadhi wa ardhioevu ya Mto Mara.

Akizungumza juzi wakati wa hafla hiyo iliyowakutani-sha wadau mbalimbali wa ulinzi wa rasilimali za Mto Mara, Mkurugenzi wa kituo cha TAFIRI-Mwanza, Dk. Baraka Sekadende, alisema dhana hizo halali za uvuvi zimegharimu zaidi ya Sh. milioni 14.6.

"Baada ya kubaini kuwapo kwa shughuli za uvuvi haramu uliokithiri kwa kushirikiana na wafadhili wa mradi huu Darwin Initiative tukaanza kampeni ilioenda sambamba na utolewaji wa elimu juu ya madhara ya uvuvi haramu na kufanikiwa kupata idadi hii ya wavuvi walioreshesha nyavu zao na kukabidhiwa mpya ambazo ni halali," alisema, Dk. Sekadende.

Aidha, alisema licha ya

kampeni bado wapo wavuvi wengine ambao wamekaidi kusalimisha nyavu haramu kwa kuogopa kuwa endapo wakizsalimisha watakamatwa dhana ambayo sio ya kweli.

Kadhalika alisema ardhi oevu ya Bonde la Mto Mara lenye ukubwa wa kilometra 387 za mraba inahitaji kuitunza na kuilinda kutoptana na miongoni mwa ardhi oevu kubwa kusini mwa jangwa la Sahara.

Mkuu wa wilaya hiyo, Juma Chikota alitoa siku 14 kwa wavuvi wote wanaojihusisha na shughuli za uvuvi haramu susani ambao hawakusalimisha dhana zao kuzsalimisha kwa hiari kabla ya hatua kali za kisheria.

Aidha, alimuagiza Ofisa Uvuvi wa wilaya hiyo kuandaa vikao na wavuvi wote ili ku-

waelimisha madhara ya uvuvi haramu pamoja na fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali ikiwamo mikopo ya serikali kuu ili kufanya uvuvi kuwa na maslahi.

Ofisa Uvuvi Wilaya ya Ranya, Godfrey Bwathondi, alisema upande wa wilaya hiyo mto huo una wavuvi 668 na 340 wanatumia zana haramu za uvuvi hivyo kuomba wadau kuendelea kushirikiana na serikali kudhibiti vitendo hiyo.

"Hizi dhana zinauzwa hadi hapa kijiji kwa bei nafuu sasa ni vyema serikali kuanzia ngazi za vijiji hadi wilaya kuweka jitihada kudhibiti na kutoomeza biashara hii ili dhana hizi zisipatikane kabisa," alisema Maendeka John, mmoja wa wavuvi.



Mkuu wa Wilaya ya Ranya, Juma Chikota (mwenye suti ya bluu) akiongoza shughuli ya uteketezaji wa zana za uvuvi haramu zilizokuwa zikitumika katika ardhi oevu ya Mto Mara na kusalimishwa kwa hlari hivi karibuni na wavuvi zaidi ya 50 katika kijiji cha Kwibuse wilayani Ranya. **PICHA: MATHIAS MARWA**

*‘Mizani kwenye minada ya mifugo ni lazima si hiari’ *

Na Yohana Shida, Geita

BODI ya Nyama Tanzania imejipanga kupeleka mizani kwenye minada kwa ajili ya kupima mifugo kabla ya kuuzwa na kununuliwa, ili thamani yake iendane na uzito halisi wa mifugo hiyo.

Ofisa Mifugo kutoka Bodii ya Nyama Tanzania - Kanda ya Ziwa, Nemesius Mukalaza alisema hayo juzi mjini

Geita katika kikao maalumu cha watalamu wa mifugo kutoka halmashauri za kanda ya ziwa.

Mukalaza alisema hatua hiyo inalenga kuondoa biashara ya makadirio na kuepuka wanunuzi ama wauzaji husasani wafugaji kuuza mifugo kwa hasara.

“Ni mojawapo ya takwa la kisheria kwamba ng’ombe wauzwe kwa uzito, wafanyabiashara wenzetu

wamekuwa wakihangaika sana kununua ng’ombe kwa makadirio. Hii inasababisha mfanyakibashara akapata faida yule muuzaji au anayeuzza ng’ombe akapata hasara ambaye mara nyingi ndio mfugaji,” alisema.

Alisema mizani pia itasaidia kupata ng’ombe wanaostahili kuingia kwenye machinjio kwa ajili ya kuchinja lakini pia nyama

bora na salama inayokidhi ubora wa kuingia kwenye soko la ndani na nje ya nchi.

Mukalaza alizitaka halmashauri kuongeza usimamizi na uboreshaji wa miundombinu kwenye machinjio ili kuimarisha usalama na ubora wa nyama na kupunguza hatari mlipuko wa magonjwa kwa binadamu.

“Machinjio zetu nyingi ambazo zinamilikiwa na

halmashauri nyingi nyingi zinakosa vigezo vinavyostahili, zina mapungufu ambayo ni mengi yanayopunguza ubora wa nyama”, alifafanua

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji mkoa wa Geita, Dk Elvis Msenya alisema Geita ina mifugo ipatayo milioni 6.42 kati yao ng’ombe ni milioni 1.1, mbuzi 497,000, kondoo 100,000 na punda 5,423.